**HOTUBA YA MHESHIMIWA HAMZA S. JOHARI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KWENYE MKUTANO MKUU WA CHAMA CHA MAWAKILI WA SERIKALI TAREHE 13 JULAI 2026 KATIKA UKUMBI WA KIMATAIFA ARUSHA**

---

**Mgeni Rasmi, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**
**Viongozi wote mliopo;**
**Mawakili wenzangu wa Serikali;**
**Mabibi na Mabwana;**
**Itifaki imezingatiwa.**
**KAZI NA UTU!....**

**Mheshimiwa Rais;**
Nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kufika hapa siku ya leo tunapokutana kwenye Mkutano Mkuu wetu wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania. Mkutano huu unakuwa wa nne tangu ulipozindua Chama hiki kule Dodoma mnamo tarehe **29 Septemba, 2022**.

Kipekee, nikushukuru sana Mhe. Rais kwa uongozi wako thabiti na kwa namna ambavyo unasimamia maendeleo ya kiuchumi, uwekezaji, amani na usalama pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kitaifa na kimataifa. Nitumie hadhara hii pia, kukushukuru kwa dhati ya moyo wangu, kwa imani yako kwangu na kuniteua kwa awamu nyingine tena kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahadi yangu kwako ni kuchapa kazi kwa bidii ili kukusaidia kuwatumikia wananchi wetu.

**Mheshimiwa Rais;**

Nawashukuru sana viongozi wetu Wakuu kutoka mihimili ya Dola, viongozi wengine wote na waalikwa kama walivyotambulishwa, kwa kukubali mwaliko wetu na kuungana nasi katika Mkutano huu. Sina maneno mazuri zaidi ya kusema **asanteni na karibuni sana.**

Nakushukuru Ndugu Samwel Maneno, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Chama cha Mawakili wa Serikali na Kamati zote ambazo zimefanikisha Mkutano huu.

**Mheshimiwa Rais;**

Siku ya leo ni siku ya kihistoria kwa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania. Historia itabaki kukumbuka kuwa wewe ndiye uliyekizindua Chama hiki jijini Dodoma. Kitendo hicho hakikuwa tu uzinduzi wa Chama kipya cha kitaaluma, bali ilikuwa ni hatua ya kimkakati ya kuimarisha taaluma ya sheria serikalini na kujenga mshikamano wa Mawakili wa Serikali nchini. Tangu ulipokizindua Chama hiki, kimeendelea kukua na kuimarika. Kimekuwa jukwaa muhimu la kubadilishana uzoefu wa kitaaluma, kujenga uwezo wa wanachama wake, kuimarisha maadili ya kazi, na kukuza ushirikiano miongoni mwa Wanasheria wa Serikali wanaotekeleza majukumu yao katika taasisi mbalimbali za umma.

**Mheshimiwa Rais;**

Tunafahamu na kuthamini sana jinsi ambavyo umekuwa ukitambua mchango wa Mawakili wa Serikali katika ujenzi wa Taifa letu. Katika siku ya uzinduzi huo, ulitubatiza Mawakili wa Serikali kuwa sisi ni **" Walinzi wa Kalamu**." Naomba kunukuu maneno yako ambayo mpaka sasa yanaendelea kuishi katika mioyo ya Mawakili wa Serikali;

> ***"Ninyi Mawakili wa Serikali, ndiyo majeshi ya kulinda uchumi wetu, kisheria uchumi wetu lazima ulindwe, uwekezaji lazima ulindwe, biashara lazima zilindwe na walinzi wa hayo ni ninyi. Ninyi ni Walinzi wa Kalamu na sheria zenu na siyo walinzi wa Bunduki''***.

Hakika, tunajivunia sana jina hili kwani lina maana kubwa sana kwetu. Askari hulinda mipaka ya nchi kwa silaha; sisi maaskari wa kalamu tunalinda uchumi,

uwekezaji na biashara kwa kutumia kalamu. Tunayatekeleza haya kwa mujibu wa sheria, kwa weledi, kwa uadilifu na kwa hoja.

**Mheshimiwa Rais;**

Malengo makuu ya Mkutano huu ni kutoa fursa kwa wanachama kujadili masuala mbalimbali yanayohusu chama chetu, maendeleo ya sekta ya sheria kwa ujumla pamoja na kufanya uchaguzi wa viongozi wa Chama cha Mawakili wa Serikali. Kauli mbiu ya Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali mwaka huu ni: **"Haki, Wajibu na Utawala wa Sheria ni Msingi wa Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050"**

**Mheshimiwa Rais,**

Ijumaa tarehe 10 Julai, 2026 tulizindua Kitabu kinaitwa **Falsafa ya Sheria ya Mama Samia: Utekelezaji wake katika Mageuzi ya Kiuchumi na Kijamii**. Kitabu kimeandikwa, kupitiwa na kuhakikiwa na timu ya waandishi na wahariri wenye uwezo wa kuchambua sheria na matokeo ya maendeleo kwa pamoja, ambayo iliongozwa na **Prof. Ambrose T. Kessy**, ambaye ni msomi, mtafiti na mtaalamu wa utawala wa umma na sera. Wazo la Kitabu lilizaliwa kutokana na tafakari ya kina kuhusu mwelekeo wa uongozi wako wa Awamu ya Sita. Tulijiuliza: katika kipindi hiki cha uongozi, sheria imetumika kwa namna gani kuleta mageuzi? Je, kuna mantiki inayounganisha marekebisho ya sheria, mabadiliko ya sera, maboresho ya taasisi na matokeo ya kiuchumi na kijamii? Je, tunaweza kueleza kwa ushahidi kwamba sheria imeanza kutumika zaidi kama chombo cha maendeleo na si chombo cha udhibiti pekee?

Maswali hayo ndiyo yalizaa wazo la **Falsafa ya Sheria ya Mama Samia**. Tuliona kuwa katika Awamu ya Sita, kuna mwelekeo unaojitokeza wazi: kutumia sheria, sera, taasisi na mifumo ya utekelezaji kujenga mazingira ya maridhiano, uwekezaji, uwazi, huduma, haki, na maendeleo ya wananchi. Mwelekeo huu haukuonekana katika sekta moja tu. Umeonekana katika kodi na mapato, uwekezaji, nishati, ardhi, TEHAMA, utalii, elimu, msaada wa kisheria, hifadhi ya

jamii, utawala bora, PPP na maeneo mengine mengi. Ndiyo maana tuliona ni muhimu kuweka mwelekeo huu katika kitabu, ili uweze kusomwa, kuchambuliwa, kukosolewa, kuboreshwa na kutumika kama rejea ya sera na sheria.
Kitabu cha Falsafa ya Sheria ya Mama Samia hakikuandikwa kama maandiko ya sifa. Kiliandikwa kama kazi ya uchambuzi. Wazo letu halikuwa kusema kuwa kila jambo limekamilika. Wazo letu lilikuwa kuchunguza kama mageuzi ya kisheria na kisera yaliyofanyika tangu Machi 2021 yanaonyesha mfumo unaoweza kueleweka, kupimwa na kujadiliwa kitaaluma. Tulitaka kuhamisha mjadala kutoka kwenye kauli za jumla kwenda kwenye ushahidi. Kwa maneno mengine, tulitaka kuuliza: sheria imebadilishwa, lakini matokeo yake ni nini? Sera imetangazwa, lakini imeleta nini? Taasisi imeanzishwa au kuimarishwa, lakini imeongeza ufanisi gani? Bajeti imetengwa, lakini imemfikia nani?

**Mheshimiwa Rais**,
Kwa mtazamo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hoja hii ni muhimu sana. Kwa mujibu wa majukumu yetu ya kikatiba na kisheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina wajibu wa kuishauri Serikali kuhusu masuala ya sheria, mikataba, utungaji wa sheria, tafsiri ya sheria, na kulinda maslahi ya umma. Lakini wajibu huo haupaswi kueleweka kwa mtazamo finyu wa kisheria pekee. Ushauri wa sheria una thamani zaidi pale unaposaidia Serikali kufanya maamuzi yanayolinda maslahi ya taifa, yanayoleta maendeleo, yanayopunguza migogoro, yanayovutia uwekezaji na yanayowezesha wananchi kupata haki kwa wakati na kupata huduma bora.

Ndiyo maana tuliiona dhana ya **Falsafa ya Sheria ya Mama Samia** kama dhana yenye maana pana. Inatukumbusha kwamba sheria si maandishi tu. Sheria ni miundombinu ya taifa. Sheria ikiandikwa vibaya, inaweza kuchelewesha maendeleo. Sheria ikiwa na utata, inaweza kuongeza migogoro. Sheria ikiwa nzito kupita kiasi, inaweza kukatisha tamaa uwekezaji na biashara. Sheria ikiwa dhaifu, inaweza kuruhusu matumizi mabaya ya mamlaka na upotevu wa rasilimali. Lakini sheria ikiwa nzuri, wazi, inayotabirika na inayotekelezeka,

inaweza kuwa msingi wa uchumi imara, taasisi zenye uwezo, wananchi wenye haki na jamii yenye amani.

Hoja zinazojadiliwa katika Kitabu cha Falsafa ya Sheria ya Mama Samia zinaakisi kauli mbiu ya Mkutano wetu. Ni kwa msingi huo, ndo maana nimeona nitoe hotuba yangu kwa kuishabihisha na Kitabu nilichokirejea. Utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 unahitaji upatikanaji wa haki, watu kuwajibika na utawala wa sheria.

**Mheshimiwa Rais,**

Katika ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za Kitabu, tulisisitiza mambo matatu. Kwanza, kutofautisha kati ya matamko ya sera na matokeo ya utekelezaji. Pili, kutofautisha kati ya miradi iliyotangazwa, miradi iliyosajiliwa na matokeo halisi. Tatu, kuonyesha changamoto pamoja na mafanikio. Kwa maana hiyo, kitabu hiki hakikusudiwi kuwa taarifa ya sherehe. Ni andiko la uchambuzi wa sera na sheria.

**Mheshimiwa Rais,**

Kitabu cha Falsafa ya Mama Samia kimetumia mbinu ya kuchanganya nyaraka, takwimu na uchambuzi wa kitaasisi na vyanzo kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali na kimepangwa katika sura zinazounganisha nadharia, sheria, takwimu na matokeo. Sura ya mwisho ya kitabu inatoa mapendekezo na hitimisho kuhusu namna sheria inaweza kuendelea kutumika kama chombo cha maendeleo.

Katika kitabu hiki, moja ya hoja tunazosisitiza ni kwamba **sheria lazima ipimwe kwa matokeo**. Haitoshi kusema kwamba sheria imetungwa. Lazima tuulize: imeongeza nini? Imeboresha nini? Imefungua fursa gani? Imeondoa kikwazo gani? Imeongeza uwajibikaji gani? Imefanya huduma zipatikane kwa wananchi wangapi? Huu ndio mtazamo wa sheria kama chombo cha maendeleo.

**Mheshimiwa Rais,**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kama Taasisi muhimu katika kuunganisha sheria na maendeleo haiwezi kubaki kuwa ofisi ya kutoa maoni ya

kisheria kwa njia ya kawaida pekee. Lazima iwe kitovu cha kuhakikisha kuwa Serikali inaingia kwenye mikataba bora, inalinda rasilimali za Taifa, inapunguza migogoro ya kisheria, inaimarisha ubora wa sheria, upatikanaji wa haki na inasaidia kujenga mazingira bora ya uwekezaji na huduma pamoja na maendeleo ya kiuchumi.

Ndiyo maana, kama Ofisi, ili kuyafikia malengo ya Dira 2050, tutaendelea kusisitiza mambo kadhaa. Kwanza, ubora wa utungaji wa sheria. Sheria lazima ziwe wazi, zenye mantiki, zinazotekelezeka na zinazolinda maslahi ya umma. Pili, usimamizi wa mikataba ya Serikali. Mikataba lazima iwe na thamani kwa Taifa na izingatie uwiano kati ya kuvutia uwekezaji na kulinda maslahi ya wananchi. Tatu, matumizi ya TEHAMA katika huduma za kisheria. Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (OAG MIS) na mifumo mingine ya kidijitali ni muhimu katika kuongeza uwazi, kasi na ufanisi. Nne, kujenga uwezo wa mawakili wa Serikali. Mawakili wa Serikali lazima wawe na uwezo wa kuelewa sheria, uchumi, teknolojia, mikataba ya kimataifa, uwekezaji “Geopolitics” na masuala ya sekta mpya.

**Mheshimiwa Rais,**
Kitabu cha Falsafa ya Mama Samia kinatukumbusha kuwa falsafa nzuri lazima ikubali changamoto. Kwa hiyo, moja ya nguvu za kitabu hiki ni kwamba hakisemi kuwa kila kitu kimekamilika. Kimeonyesha changamoto katika uratibu wa taasisi, utekelezaji wa baadhi ya sheria, mzigo wa kodi na tozo kwa baadhi ya makundi, migogoro ya ardhi, changamoto za TEHAMA, tofauti kati ya maeneo ya mijini na vijijini, uhitaji wa data bora, na changamoto za kufanya mageuzi kuwa endelevu. Hii ni muhimu. Serikali inayojifunza haiogopi kuona changamoto. Inaona changamoto kama mwaliko wa kuboresha.

Kwa hiyo, kitabu hiki kinapendekeza mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa mageuzi ya sheria na sera. Hili ni pendekezo muhimu sana. Kila sheria kubwa au mageuzi makubwa ya kisera yanapaswa kuwa na viashiria vya matokeo. Tuulize: sheria

hii imeleta mabadiliko gani baada ya miaka miwili? Baada ya miaka mitano? Imeongeza uwajibikaji? Imeongeza mapato? Imeongeza uwekezaji? Imeongeza haki? Imeondoa urasimu? Imeleta changamoto mpya? Inahitaji marekebisho gani? Huu ndio utamaduni wa kisasa wa kutunga na kutekeleza sheria.

**Mheshimiwa Rais,**

Kwa mtazamo wangu, kitabu cha Falsafa ya Mama Samia kina ujumbe kwa makundi mbalimbali:

Kwa watunga sera; ujumbe ni kwamba sheria na sera lazima zitokane na ushahidi na lazima zipimwe kwa matokeo.

Kwa mawakili wa Serikali, ujumbe ni kwamba taaluma yetu ina wajibu wa moja kwa moja katika maendeleo ya Taifa.

Kwa sekta binafsi, ujumbe ni kwamba Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya biashara, lakini biashara nazo lazima ziheshimu sheria, zilipe kodi kwa uadilifu na zishiriki katika maendeleo.

Kwa vyuo vikuu, ujumbe ni kwamba tafiti za sheria na sera zinahitajika zaidi kuliko wakati mwingine wowote.

Kwa wananchi, ujumbe ni kwamba sheria ni mali yao. Sheria ipo kwa ajili ya kulinda haki zao, kufungua fursa na kuboresha maisha yao. Sheria ina thamani pale inapobadilisha maisha ya watu.

**Mheshimiwa Rais,**

Katika awamu yako ya uongozi, tumeshuhudia namna ambavyo utoaji wa haki umeimarika, niruhusu niyataje machache:

i. Ongezeko kubwa la Majaji, Mahakimu, Mawakili wa Serikali, Mawakili wa Kujitegemea na Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria;
ii. Maboresho ya Muundo mpya wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Muundo wa Mawakili wa Serikali kwa nchi nzima;
iii. Ongezeko la vitendea kazi;
iv. Kuidhinishwa kwa miswada kuwa sheria, urekebu na ufasiri wa sheria mbalimbali;
v. Uanzishwaji na uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA na teknolojia katika utoaji wa huduma za utoaji haki na za kisheria kwa ujumla;

vi. Ujenzi wa Majengo ya Taasisi na Idara za utoaji haki, kama Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali nk;
vii. Uboreshaji wa Maslahi;
viii. Utolewaji wa Huduma za Msaada wa kisheria bure kwa Wananchi;

**Mheshimiwa Rais,**

Kwa mara nyingine tena, napenda kukushukuru Mhe. Rais. Uongozi wako katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali unahusiana moja kwa moja na hoja ya kitabu cha Falsafa ya Sheria ya Mama Samia. Sheria zikitungwa, zinahitaji kusimamiwa. Sera zikitangazwa, zinahitaji utekelezaji. Bajeti zikipitishwa, zinahitaji matokeo. Kwa hiyo, uwepo wako hapa unaunganisha fikra za kitabu na utekelezaji wa Serikali.

Kwa upande wetu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kuratibu na kushirikiana na wadau wote katika kuboresha sheria, kusimamia upatikanaji wa haki kwa wakati, kuimarisha ushauri wa kisheria kwa Serikali, kusimamia mikataba, kupunguza migogoro, na kuhakikisha kuwa sheria zetu zinaendelea kuwa chombo cha maendeleo ili hatimaye malengo ya Dira 2050 yaweze kufikiwa. Pia tutaendelea kuunga mkono tafiti, machapisho na mijadala inayosaidia kuboresha utungaji na utekelezaji wa sheria ili kuhakikisha kila mtu anapata haki kwa wakati, kila mtu kwa nafasi yake anawajibika ipasavyo na utawala wa sheria unaendelea kuzingatiwa.

**Mheshimiwa Rais ;**

Chama cha Mawakili wa Serikali kimeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 16A (1) cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268. Chama hiki ulikizindua tarehe 29 Septemba 2022 kikiwa na jumla ya wanachama wapatao 2,652. Hadi sasa wanachama hai wameongezeka na kufikia takriban 4000.

Chama hiki ni zao lako wewe mwenyewe na tunakushukuru na kukuombea dua kwa kuanzisha Chama ambacho kinawagusa wananchi moja kwa moja bila kuwatoza pesa yoyote kwa huduma zitolewazo.

**Mheshimiwa Rais;**

Tangu kuzinduliwa kwa chama hiki tumepata mafanikio yafuatayo:

i. Kutolewa Waraka wa idhini ya malipo ya posho na stahiki za Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria wanaotekeleza majukumu yao katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi za Umma, Wakala wa Serikali na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI). Kwa mujibu wa Waraka huo, kuanzia tarehe 1 Julai 2024, Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria wanapaswa kulipwa posho na ada mbalimbali ikiwemo posho ya vazi maalum kwa Mawakili *(Court Attire Allowance),* posho ya usaidizi wa pango *(Rent Housing allowance),* ada ya Chama cha Mawakili wa Tanganyika (TLS), ada ya Kamishna wa Viapo wa Mahakama Kuu na zile za chini yake kwa Mawakili walioapishwa na Mahakama, ada ya Chama cha Mawakili wa Serikali (TPBA) na posho ya simu kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Waraka huo. Nitumie fursa hii kuishukuru Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa hatua hiyo.

ii. Serikali imekiwezesha Chama kwa kiasi cha TZS 1,000,000,000.00 (Bilioni Moja).

iii. Wizara ya Katiba na Sheria imeahidi kukipatia chama Ofisi.

iv. Chama kimekuwa daraja muhimu kati ya Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), OR-TAMISEMI na mamlaka nyingine ambazo Wanachama wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria. Hatua hii imesaidia kuwafikishia Wanachama miongozo mbalimbali inayotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na ile inayotolewa na Mamlaka nyingine zenye dhamana ya kufanya hivyo kuhusiana na upatikanaji wa huduma za kisheria kwa urahisi.

Kufikia tarehe 25 Mei, 2026, idadi ya Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria walioajiriwa katika utumishi wa umma na kusajiliwa katika Daftari la Mawakili wa Serikali hadi tarehe 29 Mei 2026 ni 3,409. Chama kilizaliwa mikononi mwako, ukakilea kwa kukipa ruzuku ya Serikali, Chama kimekua na sasa kinaanza kusimama.

**Mheshimiwa Rais,**

Kwa kumalizia, napenda kurejea ujumbe mkuu wa kitabu nilichokielezea hapo juu: **sheria ina thamani pale inapobadilisha maisha ya watu.** Sheria ina thamani pale inapoongeza haki, inapolinda utu, inapofungua fursa, inapoongeza uwajibikaji, inapovutia uwekezaji, inapoongeza mapato ya Serikali, inapoboresha elimu na afya, inapofikisha nishati kwa wananchi, inapolinda taarifa zao, inapopunguza migogoro na inapojenga imani kati ya Serikali na wananchi.

Mlengo huu wa kifalsafa unaakisi nukuu ya Mchumi mmoja aitwaye Douglass North ambaye alisema;

"*Investment flourishes where laws are fair*". Tafsiri isiyo rasmi;Uwekezaji huweza kushamiri pale ambapo sheria ni za haki.

Hii ndiyo maana pana ya Falsafa ya Sheria ya Mama Samia. Ni wito wa kuifanya sheria iwe hai. Ni wito wa kuifanya sheria iwe daraja la maendeleo. Ni wito wa kuhakikisha kuwa kila sheria tunayotunga au kurekebisha inaleta matokeo yanayoonekana kwa wananchi. Ni wito wa kuifanya sheria iguse na kubadilisha maisha ya watu.

**Mheshimiwa Rais**,

Kwa heshima kubwa, napenda kukushukuru kwa mara nyingine kwa kukubali kuwa nasi leo na kwa kuja kuwa Mgeni Rasmi katika Mkutano wetu huu.

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**